

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

Simu (+255 623 185 393)  
Fax Namba: (022) 2129249



Ghorofa ya 5 Jengo la Wizara ya  
Mambo ya Ndani ya Nchi,  
9 Barabara ya Ohio,  
S. L. P 79429,  
11483 DAR ES SALAAM.

Barua pepe: [tpfcs\\_phq@tpf.go.tz](mailto:tpfcs_phq@tpf.go.tz)  
[ceo.tpfcs@tpf.go.tz](mailto:ceo.tpfcs@tpf.go.tz)

Kumb. Na: TPFCS/81/VOL. I/132

23 Oktoba, 2024

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali La Jeshi La Polisi kupitia kampuni ya Shirika ya Ulinzi (URA SECURITY) anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye Sifa na Uwezo wa kujaza nafasi kama ifuatavyo;

**1.ULINZI (Nafasi 3000)**

**A) SIFA ZA MUOMBAJI**

- Awe Mtanzania mwenye umri kati ya 18-55.
- Awe na Elimu kwanzia darasa la saba na Kuendelea.
- Awe ni raia wa Tanzania kwa uthibitisho wa cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au hati ya kusafiria
- Awe na uwezo wa kusoma, kuandika na kuongea kwa ufasaha lugha ya kiswahili.
- Asiwe na tuhuma yoyote Mahakamani au kuwahi kuhukumiwa kwa kosa la jinai
- Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atakayopangiwa
- Awe na afya njema (utimamu wa mwili)
- Asiwe na michoro (tattoo) yoyote katika mwili wake

**B) MAJUKUMU YA KAZI ZA WALINZI (SECURITY GUARDS)**

- Kuhakikisha usalama wa watu na mali zilizopo eneo la kazi
- Kuzuia vitendo vya uhalifu sehemu ya kazi
- Kuzuia wizi na majanga ya moto eneo la kazi
- Kufanya doria eneo atakalopangiwa
- Kusimamia eneo la kupaki magari lililopo eneo la kazi
- Kutoa huduma nzuri kwa mteja eneo la kazi
- Pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na uongozi

**C) VITU VINAVYOHITAJIKA KWENYE MAOMBI YA KAZI**

**I. Muombaji awe na:**

- (i) Barua ya Mkono ya Muombaji kazi.
- (ii) Barua ya utambulisho kutoka serikali za Mitaa.
- (iii) Kivuli cha Kitambulisho cha Taifa au Namba ya utambulisho (NIN) (NIDA/MPIGA KURA).
- (iv) Vivuli vya Vyeti vya mafunzo ya JKT/JKU/MG, na passport size moja iliyopigwa hivi